# MILAMBO CO - OPERATIVE UNION LIMITED

**MILAMBO CU (2018) LTD - REG. NO AFF-TBR-URA-DC-2023-57**

Telegraph: 'MILAMBO'
Tel:
Mob: 255765-567-584
Fax:

E-Mail:
*milambocultd@gmail.com*

Bomani Road,
P.O. Box 186,
**URAMBO.**

*Unapojibu tafadhali taja:*
**Kumb. Na. AB.194/199/02/VOL.I/014** 11 Februari, 2026

Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Milambo CU Ltd,
S.L.P 186,
**URAMBO.**

**YAH: TANGAZO LA MKUTANO MKUU WA NANE (8) WA MWAKA WA CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA MILAMBO UTAKAOFANYIKA TAREHE 05 MACHI, 2026.**

Tafadhali Rejeeni somo tajwa hapo juu.

Mwenyekiti wa Bodi ya Chama Kikuu cha Ushirika Milambo ameniagiza kuwatangazia kuwa Mkutano Mkuu wa nane (8) wa Milambo CU Ltd wa Mwaka utafanyika tarehe tajwa hapo juu siku ya **Alhamisi kuanzia saa 2:30 Asubuhi** katika Ukumbi wa **Roman Katoliki – WILAYANI URAMBO.**

**Ajenda za Mkutano Mkuu wa Mwaka ni:-**

1. Kufungua Mkutano
    i. Kusoma Tangazo la Mkutano Mkuu
    ii. Kusoma masharti yahusuyo Mkutano Mkuu na kuthibitisha Akidi
2. Kuchagua Mwenyekiti wa Mkutano
3. Kuthibitisha Ajenda za Mkutano Mkuu
4. Kupokea wanachama wapya na kutoa vyeti kwa wanachama waliokamilisha mafungu (Hisa).
5. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa Mkutano Mkuu uliopita
6. Kuwasilisha yatokanayo na Mkutano Mkuu uliopita
7. Kusoma na kujadili taarifa ya mkaguzi wa nje (COASCO)
8. Taarifa ya maendeleo ya shughuli za chama

9. Kusoma na kupitisha makisio ya mapato na matumizi ya mwaka wa fedha wa 2026/2027.
10. Kuteuwa mkaguzi wa nje kwa mwaka wa fedha wa 2025/2026
11. Mengineyo kwa idhini ya mwenyekiti
12. Kufunga Mkutano.

Wajumbe watakaohudhuria Mkutano huo ni wawili (2) kutoka kila Chama Mwanachama na wawe waliochaguliwa kuwakilisha vyama vyao katika Mkutano Mkuu wa Union (Mwenyekiti wa Chama cha msingi na Mjumbe mwakilishi).

Makatibu Meneja wa kila Chama Mwanachama wanakaribishwa kushiriki Mkutano kama waalikwa na **wagharamiwe na vyama vyao.**

***Zingatieni:*** *(i)* ***Kwa kuzingatia mabadiliko ya hisa za uanachama, vyama ambavyo havijahuisha hisa zao na kufikia nusu ya hisa havihusiki na tangazo /mualiko huu.***

*(ii)* ***Wanachama watakaoshindwa kukamilisha mafungu yote ya hisa ndani ya miaka 2 mfululizo (miezi 24) watakuwa wamepoteza sifa za uanachama.***

(iii) ***Kwa Mwanachama mwenye mengineyo; ayawasilishe kwa barua ofisi ya Meneja Mkuu siku 14 kabla ya tarehe ya Mkutano Mkuu kufanyika.***

**"Pamoja na Salamu za Ushirika"**

Innocent Josephat Tibesigwa
**KAIMU MENEJA MKUU.**

MILAMBO CO-OPERATIVE UNION LIMITED
REG No. AFF-TBR-URA-DC-2023-057
P.O. Box 186
URAMBO

**NAKALA KWA:-**

1. Mrajis na Mtendaji Mkuu,
   Tume ya Maendeleo ya Ushirika,
   S.L.P.201,
   **DODOMA.** – Unaombwa kuhudhuria

2. Mrajis Msaidizi (M),
   Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,
   S.L.P.25,
   **TABORA.** - Unaombwa kuhudhuria

3. Afisa Ushirika (W),
   Halmashauri ya Wilaya ya Urambo na Kaliua - Mnaombwa Kuhudhuria